


MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI, 2022) KWA MKOA WA KUSINI, PEMBA
Umetolewa: (17/02/2022)

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika mkoa wa Kusini na wilaya zake.

(I) Ngazi ya Mkoa



Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Masika, 2022 kwa kisiwa cha Pemba. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Masika katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Pemba.
Angalizo: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Machi hadi Mei, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

Dondoo

- Kwa ujumla mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini Pemba.
- Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.
- Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2022.
- Vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa kujitokeza hususan katika mwezi Mei, 2022.

Mvua za msimu wa Masika, 2022

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya wilaya za mkoa wa Kusini Pemba. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022 na kuisha wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2022.


Angalizo:

Izingatiwe kuwa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani hivyo matukio ya vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na upepo mkali yanatarajiwa kujitokeza.

(II) Ngazi ya Wilaya

MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI, 2022) KWA WILAYA YA CHAKE CHAKE
Umetolewa: 17/02/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Chake Chake.



Mwelekeo wa mvua za Masika Machi-Mei, 2022 kwa wilaya ya Chake Chake, Pemba.

Mvua za Msimu wa Masika, 2022 kwa Wilaya ya Chake Chake

Zitaanza: Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.

Zitaisha: Wiki ya tatu ya Mwezi Mei, 2022.

Kiasi cha mvua zinazotarajiwa: Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Chake Chake ni kati ya milimita 750 hadi 1070.

Kiwango cha juu cha mvua: Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2022.

Vipindi vya ukavu: Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2022.

Ulinganifu: Mvua zinatarajiwa kuwa za kutosha na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

Angalizo:

- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.
- Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi
Matokeo

- Hali ya unyevunyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao ya chakula na biashara kama vile mpunga, ndizi, karafuu na matunda inatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi.
- Upatikanaji wa chakula kwa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha. Hali hii itasaidia kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini.
- Mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mihogo na viazi vitamu yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu wa kupitiliza na maji kutuama mashambani.
- Wadudu waharibifu wa mazao na uharibifu wa miundombinu ya kilimo vinaweza kujitokeza.

Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.
- Wavuvi wanashauriwa kuandaa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya uvuvi yakiwemo maghala ya baridi na kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki hasa kwenye mabwawa.

Utubiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,

S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz


(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

105A – 09/19

(II) Ngazi ya Wilaya

MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI, 2022) KWA WILAYA YA MKOANI
Umetolewa: 17/02/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Mkoani.

 <p>Mwelekeo wa mvua za Masika Machi-Mei, 2022 kwa wilaya ya Mkoani, Pemba.</p>	<p>Dondoo muhimu</p> <ul style="list-style-type: none"> Mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mkoani. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2022. Hali ya unyevunyevu wa udongo na upatikanaji wa chakula cha samaki inatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi. Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.
--	--

<p>Mvua za Msimu wa Masika, 2022 kwa Wilaya ya Mkoani</p> <p>Zitaanza: Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.</p> <p>Zitaisha: Wiki ya tatu ya Mwezi Mei, 2022.</p> <p>Kiasi cha mvua zinazotarajiwa: Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Mkoani ni kati ya milimita 860 hadi 1070.</p> <p>Kiwango cha juu cha mvua: Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2022.</p> <p>Vipindi vya ukavu: Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2022.</p> <p>Ulinganifu: Mvua zinatarajiwa kuwa za kutosha na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.</p> <p>Angalizo:</p> <ul style="list-style-type: none"> Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

<p>Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi</p> <p>Matokeo</p> <ul style="list-style-type: none"> Hali ya unyevunyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao ya chakula na biashara kama vile mpunga, ndizi, karafuu na matunda inatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi. Upatikanaji wa chakula kwa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha. Hali hii itasaidia kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini. Mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mihogo na viazi vitamu yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu wa kupitiliza na maji kutuama mashambani. Wadudu waharibifu wa mazao na uharibifu wa miundombinu ya kilimo vinaweza kujitokeza. <p>Ushauri</p> <ul style="list-style-type: none"> Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Wavuvi wanashauriwa kuandaa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya uvuvi yakiwemo maghala ya baridi na kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki hasa kwenye mabwawa.
--

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

105A – 09/19